TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU



Benedict Ndomba.

# Ujio serikali mtandao majalada, barua na miadi vitakavyopungua

## • Ni huduma kielektroniki kifanisi huku gharama zikipunguzwa

PENGINE ni Watanzania wachache wanaposikia serikali mtandao (electronic government), wanaweza kuelewa ni jambo gani hasa, au kufikiria ni nini kitakachotokea.

Kwa wepesi dhana hii inahusisha kuachana na kujaza makaratasi kwa kalamu, kuwa na vyumba vya mafaili yenye vumbi au yaliyoliwa na mchwa, kuonana na maofisa wa serikali uso kwa uso na kugonga milango ya ofisi hizo ili kupata huduma, badala yake mambo hufanywa kielektroniki.

Serikali mtandao inahusisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHEMA),kuwapa huduma za umma wananchi na wengine wanaoshirikiana na serikali kufanikisha majukumu mbalimbali.

Hivyo, huduma za serikali zinakuwa mtandaoni na zinawafikia watu kielektroniki iwe kuwahudumia wananchi, wafanyabiashara,wateja mahakamani, vyuoni, kwenye taasisi na vyombo vyote vya umma na hata vya kimataifa na kikanda.

Kufanikisha jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma kunategemea kuwapo kwa sera, sheria, kanuni, viwango, miongozo na mikakati madhubuti ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA, katika taasisi zake yanazingatiwa, anasema, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA), Benedict Ndomba.

Anaiambia Nipashe kuwa usalama wa matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma, husaidia kulinda maslahi ya wananchi ambao ndiyo watumiaji wa huduma zitolewazo na serikali kielektroniki.

Anaongeza kuwa Sheria ya Serikali Mtandao Na 10 ya 2019, inataka kila taasisi ya umma kutekeleza miradi ya TEHAMA kwa kuzingatia viwango vya ufundi na miongozo inayoainishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ili kuepuka urudufu wa jitihada za Serikali Mtandao.

Ndomba anaeleza kuwa, ili teknolojia itumike serikalini lazima kuwe na usimamizi unaotoa mwelekeo wa kuhakikisha TEHAMA inayotumika, inaratibiwa na kuainisha matumizi sahihi na salama katika taasisi za umma.

Anasisitiza kwa, taasisi zote za umma kuzingatia kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao katika utendaji kazi ili kujenga mifumo yenye tija na kwamba sheria inazitaka na kuzielekeza taasisi hizo kuwasiliana na e-GA ili kushirikiana na kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanakuwa yenye tija kwao na serikali pia.

"Mamlaka ya Serikali Mtandao ipo kwa ajili ya kuhakikisha matumizi ya TEHAMA serikalini yanakuwa yenye tija na faida kwa serikali na wananchi siyo kwa ajili ya kuzibana taasisi za umma au kuzuia matumizi ya TEHAMA," alisema.

Anasema kwa kuzingatia matakwa ya sheria hiyo, taasisi yoyote ya umma inayokusudia kutekeleza mradi wa TEHAMA inatakiwa kuwasilisha andiko la mradi e-GA, kupitia tovuti ya huduma za TEHAMA serikalini ijulikanayo kama 'Government ICT Service Portal' (GISP).

Anasema andiko hilo linapaswa kuwasilishwa wakati wa hatua ya mipango ili kupata ushauri wa kitaalam na kibali kutoka mamlakani, akifafanua kuwa kwa miradi ya TEHAMA inayoendelea au iliyokamilika, taasisi za umma zinapaswa kuwasilisha taarifa zake sahihi na kamili kupitia GISP ili e-GA ipitie na kufanya tathmini ya miradi hiyo na kutoa ushauri wa kitaalamu ikiwa kuna maeneo ya kuboresha.

"Mamlaka hufanya ukaguzi wa miradi, mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa lengo la kuhakikisha usalama, ufanisi pamoja na uzingatiwaji wa viwango na miongozo ya serikali mtandao, kuleta tija katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Ili kufikia usalama wa mifumo, sheria ya serikali mtandao inaelekeza taasisi za umma kuhifadhi mifumo yao katika mazingira yaliyothibitishwa na serikali. e-GA inalo jukumu la kukagua mazingira yanayohifadhi mifumo hiyo kujiridhisha iwapo mazingira hayo yamethibitishwa serikalini," anasema.

Anaeleza kuwa, lengo ni kuhakikisha usalama na kwamba e-GA inaendelea kufuatilia kubaini taasisi zinazokiuka matakwa ya sheria katika kuhifadhi mifumo yao, anasema Ndomba.

"Sheria inasisitiza pale inapowezekana ujenzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ifanywe kwa kutumia wataalamu wa ndani, ili washiriki kikamilifu katika ujenzi na usimamizi wa miradi na mifumo ."

Vilevile anasema washiriki kuwezesha kutatua changamoto zinazojitokeza kwa haraka zaidi akieleza kuwa sheria haijazuia kutumia wataalamu wa nje au sekta binafsi katika ujenzi wa miradi ya TEHAMA isipokuwa ni lazima miradi hiyo ifuate sheria na taratibu zilizowekwa sambamba na kukidhi viwango vya serikali mtandao.

"Katika kuhakikisha matumizi salama e-GA imeandaa viwango na miongozo mbalimbali ya serikali mtandao ambayo inatoa maelekezo na taratibu zinazotakiwa kufuatwa na taasisi za umma katika matumizi mbalimbali ya TEHAMA," anasema.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Serikali Mtandao anasema miongozo hiyo, inaelekeza namna ya uundaji, ununuzi, usimamiaji na utekelezaji wa jitihada za TEHAMA, jinsi ya kulinda mifumo dhidi ya maafa, majanga au uharibifu na namna ya kudhibiti athari zinazoweza kupunguza utendaji wa taasisi za umma.

Halikadhalika, anasema inaelekeza umuhimu wa matumizi bora, salama na sahihi ya mifumo, data na vifaa vya TEHAMA serikalini yatakayowezesha mifumo kuungana na kubadilishana taarifa ili kufikia dira ya kuwa na mifumo ya serikali mtandao yenye tija na ufanisi.

"Taasisi zote za umma, zinapaswa kutumia kwa ukamilifu miongozo hii ili, kuleta mafanikio chanya katika utendaji na utoaji huduma pamoja na kuhakikisha kuwa, siri za serikali hazivuji kwa kutumia mwanya wa TEHAMA na hatimaye kufikia azma ya kuwa na Serikali ya Kidijiti, ambayo inapatikana muda wowote, mahali popote na kwa hali yeyote ya mtumiaji," anaeleza.

Meneja wa Huduma za Sheria e-GA, Raphael Rutaihwa, anasema uwapo wa sheria ya serikali mtandao na kanuni zake, unasaidia kuwezesha matumizi sahihi ya TEHAMA katika taasisi za umma, yanayopelekea kuboresha utendaji kazi na kutoa huduma bora zinazopatikana kwa urahisi na haraka, na hivyo kuwa na serikali ya kidigitali iliyo imara na endelevu.

Rutaihwa anasema, sheria hiyo inazitaka na kuzielekeza taasisi za umma zinazohusika na ujenzi wa miundombinu ya serikali kama vile barabara, reli na majengo kuhakikisha kuwa, zinawekewa mazingira wezeshi kwa ajili ya kupitisha miundombinu ya TEHAMA kuanzia wakati wa kuandaa michoro ya ujenzi.

"Ili kuhakikisha tunajenga serikali ya kidijitali, ni vema taasisi zote za umma zikazingatia Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, kanuni zake pamoja na viwango na miongozo ya Serikali Mtandao iliyopo," anasema mtaalamu huyo.